

Imani
*juu ya*
Hofu.

# Imani Juu ya Hofu

Majira ya Maajilio yanatualika kuandaa mioyo yetu kwa ajili ya kuja kwa Yesu, si kwa sherehe tu bali pia kwa tafakari. Katika simulizi ya Krismasi, hofu ni dhima inayojirudia: hekaluni, kwenye ndoto, milimani na hata kwenye nyumba za utulivu. Lakini kila mara, Mungu hatoi hukumu bali anatupa hakikisho: 'Usiogope.'

Mfululizo huu, Imani Juu ya Hofu, unatufundisha jinsi imani inavyoweza kukua hata pale tunapohisi kuogopa. Unatukumbusha kwamba Mungu yuko karibu wakati maisha yanapokuwa na mashaka, kwamba anaweza kuaminiwa wakati wa kusubiri, na kwamba hata hofu ikitushika, haihitaji kuwa na neno la mwisho.

Katika tafakari fupi fupi za mfululizo huu, tunachunguza jinsi kuchagua imani badala ya hofu kunavyotusaidia kumkaribisha Yesu kwa kina zaidi katika maisha yetu



Elizabetii:

# Kuamini wakati wa Mungu.

# 30 Novemba

Luka 1:5-25 na 39-45

Elizabetii aliishi na uchungu wa maombi yasiyojibiwa. Yeye na mumewe Zakaria walikuwa watu wa imani, wakimtumikia Mungu siku zote, kwa miaka huku ndoto ya kupata mtoto ikififia kadri muda ulivyopita. Kisha, ghafla, kila kitu kilibadilika. Malaika akawajia na kuwaambia ya kwamba wangejaliwa mtoto wa kiume, na Elizabetii akawa mjamzito.

Hatusikii mengi kuhusu hofu za Elizabetii, lakini lazima lazima walikuwa nayo. Baada ya miaka yote ya matumaini na kusubiri, je, kweli angeamini kuwa jambo hili lilikuwa linawezekana? Hata hivyo, alibaki na imani. Alitambua kwamba Mungu alikuwa akifanya jambo jipya, hata pale lisipoeleweka.

Badala ya kuishinda hofu na mashaka, Elizabeti alijibu kwa imani. Alipokuwa mjamzito, alisema: "Bwana amenitendea hili" (Luka 1:25), akimtukuza Mungu kwa furaha yake.

Baadaye, Maria alipomtembelea Elizabeti alijazwa na Roho Mtakatifu na mara moja akatambua kwamba Maria alikuwa na ujauzito amembeba Masihi aliyetarajiwa. Akamwita Maria "Mama wa Bwana wangu" (Luka 1:43). Aliweza kuona ambacho wengine wangeweza kukosa na akasema maneno ya baraka na uthibitisho.

Hadithi ya Elizabeti inatufundisha kwamba imani haimaanishi kila wakati kuwa na majibu yote. Wakati mwingine ni kushikilia kimya kimya, kumwamini Mungu hata kwa wakati usio wa kawaida, na kutambua kazi yake hata pale tusipoielewa kikamilifu.

Imani juu ya hofu inamaanisha kuchagua kuamini kwamba Mungu bado anafanya kazi, hata majibu yanapochelewa au njia mbele haieleweki. Elizabeti anatukumbusha kwamba wakati wa Mungu mara nyingi ni tofauti na wetu, lakini siyo kuchelewa kwa tumaini.

**Unamsubiri Mungu wapi sasa? Itamaanisha nini kwako kutenda kwa imani, hata bila kuwa na majibu yote?**

*Bwana, nisaidie kukuamini hata mambo yasipojibiwa kwa wakati niliotarajia. Hata ninapohisi hofu au kutokuwa na uhakika, nipatie imani ya kuamini kwamba bado unayafanyia kazi. Amina.*

# 1 Desemba

Luka 1:5-25 na 39-45, Zaburi 145

Hadithi ya Elizabeti ni ya uvumilivu wa kimya na imani ya kina. Yeye na Zakaria walikuwa waadilifu mbele za Mungu – waaminifu, wachaji na wenye maombi. Lakini kwa miaka mingi, walikuaa wenye huzuni kwa sababu ya maombi yao kutokujibiwa. Hitaji lao la kupata mtoto lilikua katika ukimya. Hata hivyo aliendelea kuamini.

Mungu alipofanikisha, kwa wakati na kwa njia ambayo hakuna aliyekuwa ametarajia, Elizabeti alitambua muujiza huo. Jibu lake halikuonyesha kutoamini au kinyongo, bali shukrani na mshangao. Alijitenga, akakaa miezi mitano bila kuonekana, labda si kwa aibu bali kwa heshima. Alimshukuru Mungu kwa maisha mapya yaliyokuwa yakikua ndani yake, na kwa neema iliyomwondolea aibu ya kutozaa miongoni mwa watu.

Elizabeti alielewa kwamba wakati wa Mungu mara chache hulingana na wetu, lakini makusudi yake siku zote ni mema. Kusubiri kwake hakukuwa bure; kulimwandaa kutambua ukuu wa Mungu katika jambo lisilotarajiwa.

Maria alipokutana na Elizabeti kumshirikisha habari za muujiza uliokuwa ndani yake, Elizabeti alijazwa na Roho Mtakatifu. Akiwa mzee kwa miaka na tajiri kwa ufahamu wa kiroho, aliona ambacho wengine wangeweza kukikosa – mkono wa Mungu haukupungua katika maisha ya Maria. Alisema maneno ya baraka na uthibitisho, akatangaza: “Heri yeye aliyesadiki ya kwamba yale Bwana aliyomwambia yatatimizwa” (Luka 1:45).

Hii ni zawadi ya imani iliyopevuka – kutambua uhusika wa Mungu na kusema maneno ya ujasiri kwa mioyo ya wengine. Katika ule wakati mtakatifu, alipokuwa sauti ya uthibitisho kwa mtu kijana aliyekuwa anaingia katika yasiyojulikana, Elizabeti anatufundisha kuona jinsi imani inayosimama na kuvumilia kupitia kusubiri inavyoweza kuwa imani inayowatia nguvu wengine, inayojenga urithi, na inayozungumza uzima kwa kizazi kijacho.

Katika dunia iliyojaa hofu na mashaka, tunahitaji sauti thabiti ya wale waliovumilia vyema na kuamini kwa kina.

**Unawezaje kusema maneno ya baraka na uthibitisho kwa vizazi vingine leo?**

*Mungu mwaminifu, asante kwa kuwa unasikia kila maombi. Kama Elizabeti, nisaidie nitambue utakatifu katika lisilotarajiwa na niongeze imani ndani ya mioyo ya wengine. Nipe macho ya kuona mkono wako ukitenda kazi na ujasiri wa kutia moyo leo. Amina.*

# 2 Desemba

Luka 1:5-25 na 39-45, Zaburi 37:1-7

Tunapotazama uzoefu wa Elizabeti, tunaona kinachowezekana tunapoendelea kumwamini Mungu, hata pale maisha yanapokwenda kinyume na matarajio yetu.

Elizabeti na Zakaria walikuwa wamepitiliza sana umri wa kuzaa. Lakini pale watu walipoona wanandoa wazee mno kuzaa na kuwa na familia yao, Mungu aliona watoto wake waaminifu na akafanya njia. Katika tendo hili la kimiujiza, tunaona nguvu zisizo na kikomo za Mungu na upendo wake mkamilifu ukiwekwa wazi. Tunakumbushwa shauku yake na uwezo wake wa kutenda zaidi ya matarajio ya kibinadamu, kuwabariki waaminifu kwa njia zisizotarajiwa.

Na huyu hakuwa mtoto wa kawaida bali ni utimilifu wa unabii wa kale – kuwasili kwa Yohana Mbatizaji, yule ambaye angeandaa njia kwa ajili ya Mwana wa Mungu, Mwokozi wa wote.

Kupitia hadithi ya Elizabeti na Zakaria, tunaona mwanga wa mpango mkubwa wa Mungu ukifunguliwa. Miaka yao ya kukatishwa tamaa na kuaibika haikuwa mwisho wa simulizi, bali sehemu ya kusudi la Mungu kwao. Maisha yao yanashuhudia nguvu ya uvumilivu katika imani na utumishi, hata kupitia vipindi vya ukimya na kusubiri. Wanatukumbusha kwamba hali inapokuwa haiwezekani, tunapaswa kutazama kwa Yeye anayeweza kufanya yote yawezekane.
Mbele ya kuchelewa, kukatishwa tamaa au mashaka, mbele ya lisilowezekana, tumeitwa kumkumbuka Mungu ni nani – Yeye aliye mwaminifu, anayependezwa na hushusha baraka zake tele kwa wale waaminifu kwake pia.

Wakati hofu inapotwambia muda unaisha, imani yetu itukumbushe kwamba Mungu hachelewi. Anaona utiifu wako. Anasikia maombi yako ya moyoni. Naye anaweza kufanya zaidi ya vile tunavyoweza kuomba au kufikiria – kwa wakati wake mkamilifu.

Tumtumikie kwa uaminifu, unyenyekevu na bidii, tukijua kwa uhakika kwamba anatuona, anatujua na atatimiza mpango wake mkamilifu kadiri tunavyoendelea kumtumainia.

**Ni sala gani umeacha kuomba kwa sababu ya subira ya iliyochukua muda mrefu mno? Inaweza kuonekanaje kuileta tena mbele za Mungu leo?**

*Bwana, ninapochoka kusubiri, nikumbushe kwamba wewe ni mwaminifu. Nisaidie kuamini wakati wako na kukutumikia kwa ujasiri wa ndani, nikijua kwamba wewe unaona, unasikia na utatenda. Amina.*

Major Rosemary Matunde

Kuamini wakati wa Mungu.

# 3 Desemba

Luka 1:5-25 na 39-45, Waebrania 11

Baadhi ya makuhani wakuu katika Biblia walilazimika kusubiri miaka mingi kwa ahadi za Mungu.

Musa alisubiri miaka 40. Kisha akawaongoza watu kwa miaka 40 zaidi. Mungu alimwomba afanye mambo ambayo alihisi hayamstahili na hakuwa na vifaa navyo. Musa hakuwahi kufika nchi ya ahadi. Lakini tazama yote aliyotimiza njiani.

Yusufu alipata maono. Lakini utumwa, gerezani na njaa vilikuwa sehemu ya mpango kabla maono hayo kuwa ya kweli. Yusufu aliendelea kuwa mwaminifu. Katika hali zisizo bora, alitumia fulsa ambazo Mungu alimjalia katika mabadiliko ya maisha njiani.

Daudi alisubiri takribani miaka 15 kuwa Mfalme wa Israeli. Alijua itatoke kwa wakati ujao. Katika kusubiri, Daudi alihisi yote, lakini alibaki mwenye shauku kuhusu wito wake, mtu aliye baada ya moyo wa Mungu. Kwa watu hawa, kama vile Elizabeti na Zakaria, maisha hayakuhitaji kusubiri. Kila kitu kilichotokea katikati kilitumika kuwaandaa, ndani na nje, kwa ajili ya kilichokuwa kinakuja. Kisha walipofikia ahadi zao, walibarikiwa kupita kipimo. Wote walikuwa na mapungufu. mashaka, waliuliza, walipotea. Lakini Mungu alikuwa na mpango. Wote walichaguliwa na Mungu kwa kusudi. Na yote katika wakati mkamilifu wa Mungu. Wote walikuwa na imani, walimjua Mungu wao ni nani na kwamba anaweza kuaminika. Walikuwa na tumaini kwa kilichokuwa kinakuja.
Kuna mifano isiyohesabika mingine, katika Biblia na pia kwa hakika katika simulizi lako pia.

Hata kama bado haujafika pale ulipotegemea kuwa, au kama unahisi bado unangoja majibu au maagizo yanayofuata, Mungu anakualika umtumainie, ukumbuke wema wake na uaminifu wake.

Mungu wetu yupo pamoja nasi, yupo kwa ajili yetu na anafanya kazi, hata tusipoona.

**Unangoja nini sasa hivi? Muombe Mungu akufunulie kile anachotaka kukufundisha unapoendelea kungoja.**

*Bwana, nisaidie kukuamini ninapo kusubiri. Nifundishe uvumilivu na uandae moyo wangu kwa ajili ya kilichopo mbele. Hata nisipoona njia, nikumbushe kwamba wewe ni mwaminifu na unafanya kazi. Imarisha imani yangu na udumishe tumaini langu. Amina.*

# 4 Desemba

Luka 1:5-25 na 39-45, Waebrania 11:1, Habakuki 2:3

Sala inaweza kufafanuliwa kama mawasiliano ya dhati na Mungu. Ni mwaliko wa kumkaribia Mungu, kwa njia rasmi au isiyo rasmi kadri tunavyotaka. Wakati mwingine tunaweza kutopata majibu ya maombi yetu mara moja, bali tunapaswa kusubiri. Mungu amepanga mambo makubwa kwa maisha yetu, naye atafanya mambo makuu zaidi katikati yetu. Tunaposubiri majibu, hofu na mashaka yanaweza kuingia ndani yetu. Katika nyakati hizo, tunapaswa kumwamini na kuwa na imani kwake. Hili ni jambo muhimu katika safari yetu ya Kikristo.

Nilipokuwa na umri wa miaka 17, nilikuwa na ndoto na makusudi mbalimbali kwa ajili ya maisha yangu ya baadaye. Kwa wakati huo yalichanganya, nilikuwa na maamuzi muhimu ya kufanya ambayo yangebadili mwelekeo wa maisha yangu. Nilikua nikilisali kwa ajili ya hizo ndoto na makusudi yake. Nikaendelea kusubiri.

Katika kipindi hicho cha kusubiri, nilihisi kana kwamba Mungu hakuwa akisikia maombi yangu. Nilitarajia kwamba angekua nami katika nyakati hizo ngumu, lakini mara nyingi nilijihisi mpweke. Hofu yangu iliendelea kwani sikuwa najua mustakabali wa maisha yangu ya mbele au ningefanya nini. Wakati mwingine, katika hali yangu ya kutokuwa na uhakika, nilijishuku. Sasa natambua kwamba hata katika kusubiri kwangu, katika wasiwasi, mashaka na hofu, Mungu aliendelea kuwa nami kimya kimya akinifanyia mambo makubwa.

Niliendelea kusali kwa sababu nilijua Mungu alikuwa na mpango kwa maisha yangu na alijua kitakachofuata. Nilishirikiana na baadhi ya viongozi wangu wa kiroho, na nilipojifunza Neno lake, Mungu aliendelea kunena nami kupitia Maandiko. Katika kusubiri, nilijifunza kuhusu uvumilivu kwa njia mpya – kwamba Mungu hufanikisha mpango wake ndani yetu, si kwa wakati tunaoutaka sisi, bali kwa wakati ulio sahihi na bora. Na tunapomngojea kwa imani, hutujibu.

Nilisubiri kwa miaka miwili ili kupata jibu. Kwa kweli, miaka miwili ilionekana kama muda mrefu sana kwangu na kusubiri kwa muda mrefu kwa jibu la Mungu kulikuwa kugumu. Lakini katika kusubiri kwangu, nilijifunza kumwamini zaidi. Kuwa na imani kwamba angenijibu. Na kweli alifanya hivyo. Jibu lilikuja na nikafanya uamuzi wangu. Labda nawe pia unakabiliwa na wakati wa kusubiri kama huu, au utakabiliana nao siku za usoni. Katika nyakati hizo, kumbuka
kubaki karibu na Mungu na kutumainia kazi yake njema. Kuwa na imani kwa Mungu, Mlinzi na Mwongozi wetu, kunaweza kupunguza hofu katika hali hizo zisizojulikana. Mwongozo wa Mungu uwe nawe leo na kesho.

**Unaweza kufanya nini ili kubaki karibu na Mungu katika nyakati za kusubiri, katika hali ambazo ni rahisi au vya kushawishi kuacha badala ya kumkaribia zaidi?**

*Baba, nisaidie kubaki karibu nawe ninaposubiri. Nifundishe kuamini wakati wako na kutoenda mbele yako. Uweke moyo wangu karibu nawe na unijaze na amani ninaposubiri mpango wako mkamilifu. Amina.*

Bethel Kumaravel

# 5 Desemba

Luka 1:5-25 na 39-45, Wagalatia 4:4, Yohana 6:35

Tangu mwanadamu alipoanguka, Mungu aliahidi ukombozi. Lakini karne zilipita kabla ya Masihi kuja. Vizazi vilisubiri kwa tumaini, katikati ya ukimya, uhamisho na hali ya kutokuwa na uhakika. Kisha, kwa wakati ulio sahihi kabisa, Yesu akaja. Si kwa nguvu au ukuu, bali kwa unyenyekevu na utulivu.

Wakati wa Mungu unaweza kuonekana wa ajabu kwetu, lakini si wa kubahatisha. Katika barua yake kwa Wagalatia, Paulo anatukumbusha kwamba Kristo alitumwa na Mungu "wakati ulipotimia kikamilifu". Si mapema mno. Si kwa kuchelewa. Kwa wakati sahihi kabisa kama Mungu alivyokusudia.

Katika maisha yetu sisi wenyewe, kusubiri kunaweza kuhisiwa kama kumesahaulika. Maombi hayajajibiwa. Ndoto zimeahirishwa.

Lakini katika maajilio inatukumbusha hili: Mungu atafanya kile alichoahidi, kwa wakati sahihi zaidi. Mipango yake inatekelezwa kwa usahihi, si kwa kusita.

Katika Yohana 6:35, Yesu anasema, "Mimi ndimi chakula cha uzima. Yeyote ajaye kwangu hataona njaa kabisa." Hii si kuhusu mahitaji ya kimwili pekee bali pia njaa ya kina ya moyo wa mwanadamu. Njaa ya kusudi, amani, uponyaji na tumaini. Yesu hutosheleza kila shauku, si kila mara kwa njia tunayotegemea, lakini kila mara kwa wakati mkamilifu.

Huenda unasubiri ufafanuzi, mafanikio au urejesho. Na ni sawa kutaja uchungu huo. Lakini usikate tamaa. Mungu anakutazama. Anajua hitaji lako. Na katika utimilifu wa wakati wake, atakupa kile kilicho bora zaidi.

**Chukua muda kidogo wa  kutafakari:  ni nininininacholisha roho yangu? Chagua njia moja ya makusudi ya kupata lishe ya kiroho kutoka kwa Mungu – kupitia Maandiko, sala, ibada au tafakari ya utulivu. Mwachie akutane nawe hapo.**

*Bwana, lisha roho yangu kwa uwepo wako na unijaze na amani yako. Nisaidie kupata utimilifu wa kweli ndani yako pekee, nikiamini kwamba wewe hutimiza kila shauku ya moyo wangu. Amina.*

# 6 Desemba

Luka 1:5-25, 39-45 na 46-54

Tunapofika mwisho wa juma la kwanza la Majilio, tunasimama kutuliza mioyo yetu na kutafakari. Leo, tunakualika ukae na Wimbo wa Maria, Magnificat, wimbo wenye nguvu wa sifa na imani. Maneno yake yanatualika kuona rehema, nguvu na haki za Mungu zikifanya kazi katika maisha yetu. Tupate ujasiri, nguvu na tumaini katika wimbo huu wa kale wa imani ambao bado una maana kubwa leo.

"Lo, roho yangu yamsifu Bwana.
Na roho yangu inamfurahia Mungu Mwokozi wangu!
Kwa kuwa amemwangalia mtumishi wake mnyenyekevu,
na tangu sasa vizazi vyote wataniniita mwenye heri.
Kwa kuwa Mwenye Nguvu ni mtakatifu,
naye amenitendea mambo makuu.
Anaonyesha rehema yake kutoka kizazi hadi kizazi
kwa wote wamchao.
Mkono wake wenye nguvu umetenda mambo makuu!
Amewatawanya wenye kiburi na majivuno yao.
Amewaangusha wakuu kutoka kwenye viti vyao vya enzi
na kuwatukuza wanyenyekevu.
Amewashibisha wenye njaa kwa mambo mema
na kuwapeleka matajiri mikono mitupu.
Amemsaidia mtumishi wake Israeli
na kukumbuka kuwa mwenye rehema."

– Luka 1:46-54 (Tafsiri mpya)

**Chukua muda kutazama nyuma katika siku chache zilizopita. Mungu amekuwa akisema nini nawe katika juma hili la kwanza la Majilio?**

*Ee Mungu mwenye neema na upendo, tunapokuwa katika majira haya ya matarajio, tuliza mioyo yetu na fungua masikio yetu. Kama vile Maria, tusaidie kutambua mkono wako ukitenda kazi – ukiwainua wanyenyekevu, ukiwalisha wenye njaa na kuonyesha rehema zako vizazi hadi vizazi. Tupatie ujasiri wa kukuamini kwa kina zaidi, nguvu za kutembea kwa imani na tumaini la kuona ahadi zako zikitimia hata sasa. Amina.*


Maria:
Wakati huielewi.

# 7 Desemba

Luka 1:26-38

Maria alikuwa binti mdogo asiye na umaarufu wowote, na ndiye alichaguliwa kubeba ujauzito wa Masihi. Si mtu ambaye yeyote angefikiria kuwa sehemu ya mpango wa wokovu wa Mungu. Lakini njia za Mungu mara nyingi huwa za kushangaza. Malaika alipomtokea na kumwambia kwamba angejifungua Masihi, Maria alichanganyikiwa kwa haki na akauliza, hili lingewezekanaje, kiasili, hilo jambo lililoonekana kutowezekana.

Swali lake halikuwa la mashaka au kutokuamini. Lilikuwa jibu la kweli la mtu aliyekuwa anajaribu kuelewa jambo lililokuwa zaidi ya ufahamu wake. Hakukimbia. Hakubisha. Wala hakuhitaji uthibitisho zaidi. Badala yake, alisikiliza. Kisha akajibu kwa imani: "Na iwe kwangu kulingana na neno lako" (Luka 1:38).

Maria hakuwa na majibu yote. Hakujua jinsi siku zake zijazo zingekuwaje, jinsi Yosefu angezipokeaje hizo taarifa ikiwa na mwitikio wa wengine pia. Lakini alimwamini Mungu vya kutosha na kusema "ndiyo".

Hadithi yake inatukumbusha kwamba imani si kinyume cha maswali. Imani ni kusema "ndiyo" kwa Mungu hata pale tunapokuwa hatuna uhakika au tunaogopa. Ni kuchagua kumwamini Mungu hata maisha yanapogeuka ghafla, kuamini kwamba Mungu anaweza kufanya kazi hata tusipoelewa kikamilifu.

Tukiwa na hofu katika Imani haimaanishi kwamba hatupaswi kuuliza "vipi". Inamaanisha tunampelekea Mungu swali letu la "vipi" na bado tunachagua kumfuata. Kama Maria, tunaweza kubeba maswali na ujasiri, tukijua kwamba Mungu yupo pamoja nasi katika yote.

**Ni lini umewahi kuhisi kuzidiwa na kile ambacho Mungu anaweza kuwa anakutaka ufanye? Inamaanisha nini kusema "ndiyo", hata katika hali ya kutokuwa na uhakika?**

*Bwana, ninapohisi hofu na kutokuwa na uhakika, nisaidie kuwa na ujasiri wa kukuambia "ndiyo". Imani yangu ikue hata katikati ya hofu yangu. Amina.*

# 8 Desemba

Luka 1:26-38, Isaya 55:8-9, Methali 3:5-6, Waebrania 11:1

Sisi ni wanadamu. Tuliumbwa kwa uzuri na kwa namna ya ajabu. Tukiwa na akili zenye mipaka na uelewa mdogo, mapungufu mengi na hofu zisizo na msingi. Lakini pia tuliumbwa kwa mfano wa Mungu, tukiwa na uwezo wa kutumaini bila kikomo, kuamini bila kuacha na kupenda kwa namna ya pekee. Na pia kuuliza maswali.

Jibu la Maria kwa mjumbe wa Mungu halihisi kuwa geni au lisilowezekana, bali la kibinadamu kabisa. Lilikuwa jibu la udadisi, lililojengwa juu ya kujiamini kwa yule ambaye Mungu wake ni nani. Hakuwa anakataa ujumbe huo; alikuwa anajaribu kuuelewa. Na katika wakati huo tunaona kitu kizuri: kwamba Mungu anakubali maswali yetu ya kweli yanapotoka katika mioyo iliyojaa imani.

Je, Mungu amewahi kukuomba ufanye jambo ambalo halikuwa na maana? Jambo lililopingana na mantiki yako au kuharibu mipango yako?

Labda upo hapo sasa hivi – umesimama mbele ya hali inayoonekana haiwezekani. Katika nyakati hizo, kama Maria tunaweza kujibu kwa udadisi wa kweli badala ya hofu au upinzani. Tunaweza kuuliza, “Hili linawezekanaje?” si kama tamko la mashaka, bali kama tangazo la imani linalomtumainia Mungu kufungua njia, hata pale tusipoiona.

Yeye hapuuzii maswali yetu: anakutana nasi ndani yake, ananena mioyoni mwetu na anatukumbusha kwamba hakuna lisilowezekana kwake.

Achilia maswali yako yakukaribishe karibu zaidi na Yeye anayeshikilia majibu yote.

Lolote lililo mbele, iwe linaeleweka au la, tuwe na ujasiri wa kuchagua imani badala ya hofu na unyenyekevu wa kusema, “Mimi ni mtumishi wa Bwana.”

**Fikiria swali ambalo umekuwa nalo moyoni mwako. Jambo ambalo hujalisema kikamilifu kwa Mungu kwa sababu linaonekana lisiloeleweka, gumu au takatifu mno. Leo, lipeleke swali hilo kwake katika sala. Usilifiche, liweke mbele yake. Kisha tumia muda kusikiliza. Acha imani yako ikue zaidi kati ya kuuliza na kuelewa.**

*Mungu, asante kwa kukubali mshangao wangu, kuchanganyikiwa kwangu na shauku yangu ya kuelewa. Nisaidie kukuamini hata mambo yasipoeleweka. Kama Maria, nipatie moyo ulio wazi, wenye udadisi na uliojaa imani. Nifundishe kusema, “Mimi ni mtumishi wako”, hata pale njia iliyo mbele isipoeleweka. Amina.*

# 9 Desemba

Luka 1:26-38, Mathayo 19:26, Luka 2:19

Hakuna lisilowezekana kwa Mungu.

Haya ndiyo maneno ambayo Gabrieli alimwambia Maria alipomshirikisha habari kuhusu mimba ya Elizabeti, ujauzito ambao haukutarajiwa kutokana na umri wake.

Maneno haya yanarudiwa na Yesu katika Mathayo 19:26: "Kwa wanadamu hili haliwezekani, bali kwa Mungu mambo yote yanawezekana."

Nimeyahifadhi maneno haya moyoni mwangu. Maarifa yetu ya kumjua Mungu ni nani na kile anachoweza kufanya hutusaidia kushinda hofu katika maisha yetu. Ninapojua Mungu ni nani, hakuna cha kuogopa, kwa sababu kwake mambo yote yanawezekana!

Nilipokuwa mtoto mdogo, nilipoteza mwanasesele wangu niliyempenda sana muda mfupi kabla ya kulala. Nilimtafuta kila mahali bila mafanikio, niliishia kusali kwa Mungu kwa shauku. Sala yangu ilisikika hivi: "Ukinisaidia sasa, nitafanya chochote unachotaka nifanye na nitakushukuru maisha yangu yote." Maneno makubwa kutoka kwa mtoto mdogo, lakini nilimwamini Mungu kwa moyo wa kitoto na alisikia sala yangu kila mara.

Inaweza kuonekana kama hadithi ndogo tu, lakini kama Maria, nimehifadhi hadithi hii moyoni mwangu, na Mungu mara kwa mara hunikumbusha ahadi niliyomuahidi. Baadaye katika maisha, aliniita kuwa afisa wa Jeshi la Wokovu, na ingawa bado mara nyingine "natembea juu ya maji" kwa imani kama ya Petro, wakati mwingine nikiwa na hofu, Mungu hunikumbusha nisiogope bali nimtumainie kwamba daima yupo kwa ajili yangu. Ninapoitwa kufanya chochote, hukubali: "Nitafanya chochote unachotaka nifanye!"

**Ni tofauti gani hutokea maishani mwangu ninapoweka tumaini langu lote kwa Mungu?**

*Baba wa Mbinguni, nakushukuru kwa kunitunza, hata ninapokuwa na hofu na sijui cha kufanya. Kama Maria, ninasalimisha maisha yangu mikononi mwako tena. Amina.*

Meja Elisabeth Grahn

# 10 Desemba

Luka 1:26-38, Luka 2:19

“Maria aliyahifadhi mambo haya yote, akiyatafakari moyoni mwake.” – Luka 2:19

Maisha ya Maria yalibadilika mara moja. Ujumbe wa mbinguni, mwito wa kiungu na njia ambayo hakuna mtu alikuwa mepitia kabla. Hakukuwa na mwongozo, wala hakukuwa na uhakikisho, hakuna mwongozo wa maelekezo wala mpango ulio wazi.

Katika dunia inayokimbilia majibu na uhakika, Maria anatualika tufanye jambo la mabadiliko: kulihifadhi fumbo. Kulikuwa na mambo mengi ambayo Maria hakuweza kuyaelewa, lakini badala ya kudai maelezo, aliweka nafasi moyoni mwake kwa ajili ya simulizi linalofunuliwa na Mungu. Alisikiliza, alitambua, alihifadhi.

Sote tumewahi kupitia nyakati maishani ambazo hazikuwa na maana kwa wakati huo. Vipindi ambavyo sala zilionekana hazijajibiwa, pia zilikuwa hazina uhakika au Mungu akatuita twende njia mpya kabisa.

Kila mara hatupati uhakika, lakini tunakuwa na chaguo. Chaguo la kufunga mioyo na kusonga mbele, au kubaki wazi, kutazama na kusubiri maagizo yanayofuata.

Kwa umbali na muda fulani, tunaweza kuanza kuona mazungumzo yaliyotuletea faraja ya utulivu, mstari wa maandiko uliorudi kwetu tena na tena, wema usiotarajiwa uliotubeba. Hayo yalikuwa ni hazina.

Kuhifadhi kitu haimaanishi kila wakati tunaelewa. Inamaanisha tunachagua kukithamini. Kukishikilia na kukitazama kwa ukaribu kwa mshangao na imani. Zoezi la kimya la Maria la kuhifadhi linatuonyesha imani inayosikiliza zaidi kuliko inavyoongea, inayotafakari zaidi kuliko kutafuta kuelewa.

Inakuaje kama Mungu anakualika si kufahamu kila kitu bali kutambua tu? Kuhifadhi kile anachofanya?

**Tafakari kidogo, maneno au uzoefu gani Mungu anakualika uyahifadhi, hata kama hayana maana kwako sasa hivi?**

*Baba mwenye upendo, nifundishe kuhifadhi uwepo wako na kukuamini katika wakati wako, hata nisipoelewa. Nibebe imani moyoni mwangu kama Maria, nikichagua kutafakari badala ya kuogopa, kushangaa badala ya kuwa na wasiwasi. Amina.*

# 11 Desemba

Luka 1:26-38, Warumi 8:28

Kuna wakati ambapo maisha hunong'ona mwito bila maelekezo ya moja kwa moja – ni kama msukumo kuelekea kitu kisichojulikana. Binafsi, naamini hapo ndipo imani inaanza kuchanua. Hadithi ya Maria inanikumbusha kwamba si lazima kila mara nielewe kikamilifu, bali niamini kikamilifu. Kumekuwa na nyakati ambapo nimehisi kusukumwa kuchagua mambo fulani ambayo hayakuwa na maana – kuitumia sauti yangu kusema pale ambapo ukimya ungelikuwa salama zaidi, au kuamini katika neema wakati kila kitu kilihisi kutokuwa na utulivu.

Nimesimama katika sehemu ambazo mipango ya Mungu kwangu ilionekana ya kuchanganya au hata ya kutisha, na kumekuwa na wakati ambapo nimechagua kupuuza mipango ya Mungu kwangu kwa sababu nilikuwa na hofu kubwa. Lakini simulizi ya Maria imenikumbusha kila mara kusonga mbele na si kurudi nyuma. Nimejifunza kwamba neema hutupata katika utiifu na si katika ufahamu. Si kila mara twaweza kuwa na majibu – bali kuwa na imani ya kutosha kusema 'ndiyo'.

Kwangu, imani juu ya hofu haimaanishi kwamba hatutatikisika. Inamaanisha tunajikita katika upendo unaofukuza hofu. Pia inamaanisha kwamba yale tusiyoelewa kwa wakati huo yanapata maana kadri simulizi linavyoendelea kufunuliwa.

**Je, umewahi kusema 'ndiyo' kwa jambo bila kujua litakupeleka wapi, na baadaye ukagundua kwamba Mungu alikuwa akiandika kitu kizuri kupitia kujisalimisha kwako?**

*Baba wa Mbinguni, wewe ujuaye mioyo yetu, asante kwa kunena katika nyakati za kawaida za maisha yetu. Kama Maria, tusaidie kusema 'ndiyo' hata tunapokuwa na hofu au hatuna uhakika. Na imani inayothamini ahadi zako ikue ndani yetu, hata njia yetu isipoeleweka. Kujisalimisha kwetu kuwe mbegu ya utukufu wako. Amina.*

Maleleko Munkombwe

# 12 Desemba

Luka 1:26-38, Isaya 55:8-9, Habakuki 1:5

Katika ubinadamu wetu, mara nyingine tunaweza kulegea kuhusu nguvu na uwepo wa Mungu wetu, bila kukusudia kupunguza matarajio yetu ya kile anachoweza kutimiza, tukipoteza mtazamo wa kazi yake inayoonekana wazi kuzunguka kwetu. Hatujikusudii kufanya hivyo, lakini taratibu na kwa siri tunaanza kutarajia kidogo. Tunaacha kutafuta ya kimiujiza, tunaacha kutarajia majibu ya maombi na kuanza kuelezea mambo yasiyoya kawaida.

Lakini tukiwa wataratibu na kuzingatia, tunaweza kuona mkono wa Mungu ukifanya kazi kwa undani katika maelezo ya maisha yetu ya kila siku. Katika upatikanaji wa rasilimali ambazo hatuna chanzo chake, katika miadi isiyotarajiwa inayotuletea rangi, uwazi au faraja kwa siku zetu, katika suluhisho la matatizo tuliyokuwa tukiyawazia kwa kukata tamaa. Hii ni ushahidi wa Mungu aliye karibu, anayehusika na aliye mwaminifu.

Tunapokuwa tumetumia muda katika uzoefu wa Maria katika siku hizi, labda kumbukumbu kuu ni hii: Mungu hupendezwa kutumia cha kawaida kutimiza kisicho cha kawaida – naye anatualika kuitikia kwa imani, hata tusipoelewa. Anatualika, kama Maria, kuweka tumaini letu si katika kujua maelezo yote au kila sehemu ya mpango, bali katika Yeye anayetuita.

Mungu alimchagua msichana wa kawaida, asiye na uzoefu, kijana, awe sehemu ya mpango wake wa ukombozi kwa ulimwengu. Maria hakuwa msomi wala kiongozi. Hakuwa na nafasi ya mamlaka au heshima. Hata hivyo Mungu alimwangalia kwa kibali na kumwita katika jambo la lisilotarajiwa.

Katika msimu huu wa Majilio, tuhamasishwe kurudi katika mshangao na heshima, kugundua tena ukuu na uweza wa Mungu wetu. Tusipoteze mtazamo wa ya kimiujiza katikati ya mambo ya kawaida na tusije tukapoteza mshangao wa kumjua Mungu wetu ni nani na kile anachoweza kufanya – Yeye anayetuita kutoka sehemu zetu za faraja, kutufuata katika yasiyojulikana, ya kutisha, kwa nguvu zake na kwa utukufu wake.

**Leo, muombe Mungu akufungue macho ya kuona uwepo wake katika maisha ya kila siku. Tafuta yasiyotarajiwa, yasiyoelezeka, yasiyoweza kupuuzwa. Na unapoyaona, jibu lako liwe la imani: "Hili linawezekanaje?"**

*Bwana, nisamehe ninapopoteza mtazamo wa mshangao wako, ninapoacha kutarajia kwamba utatenda kwa njia zenye nguvu na za kibinafsi. Fungua macho yangu kuona uwepo wako katika maisha ya kila siku, na uwashe tena ndani yangu moyo unaoona na kuamini, hata nisipoelewa. Amina.*

# 13 Desemba

Luka 1:26-38, Zaburi 40, Methali 3:5-6

“Mtumainie Bwana kwa moyo wako wote wala usizitegemee akili zako mwenyewe; katika njia zako zote mkiri yeye, naye atayanyosha mapito yako.” – Methali 3:5-6

Leo, tunakuhimiza upumzike katika uwepo wa Baba yako wa Mbinguni, Yeye anayekualika umtumainie, hata usipoelewa. Katika dunia inayohitaji uhakika kila mara, Mungu anatuita kujisalimisha. Unapopumzika leo, achilia hitaji lako la ufafanuzi na tegemea uwepo wa Baba yako mwenye upendo na mwaminifu.

**Hadithi ya Majilio imejaa fumbo, ukimya na kusubiri. Katika utulivu, Mungu mara nyingi hunena. Tenga muda leo kukaa kimya mbele za Mungu. Bila ajenda na bila maneno, sikiliza tu. Acha tendo hili la utulivu liwe tamko la ‘Siwezi kuelewa kila wakati, lakini nakutumainia.’**

*Baba, asante kwa kunialika nije kwako, jinsi nilivyo. Nisaidie nisiutegemee ufahamu wangu mwenyewe, bali nipumzike katika hekima na upendo wako. Amina.*


Yusufu:
Wakati
inakugharimu kitu.

# 14 Desemba

Mathayo 1:18-25

Yusufu alikuwa na kila sababu ya kumwacha Maria. Kwa mtazamo wake, ilikuwa kama usaliti. Mwanamke aliyeposwa naye alikuwa akitarajia mtoto ambaye hakuwa wake. Alikuwa tayari ameamua kujitenga naye kwa siri (Mathayo 1:19), njia ya kulinda heshima yake na heshima ya Maria pia. Lakini kisha Mungu akaingilia kati.

Usiku kukiwa kumetulia, malaika alimtokea akiwa na ujumbe: 'Usiogope.' Habari ya Maria haikuwa kashfa, ilikuwa mpango mtakatifu. Mungu alikuwa akifanya kazi kwa namna ambayo hakuna mtu aliyewahi kuona hapo awali. Yusufu alikuwa na chaguo la kufanya.

Uamuzi wake ulikuwa wa ujasiri na kinyume na destuli. Kuchagua kumchukua Maria kama mke wake kulimaanisha kuingia katika hukumu ya jamii, kuhatarisha heshima yake na kubeba mzigo wa jambo ambalo hangeweza kulieleza kikamilifu.

Imani yake haikuwa tu imani ya moyoni – ilikuwa utiifu wa ujasiri mbele ya kutokueleweka. Hakuiruhusu hofu iamue mustakabali wake. Badala yake, aliyaunganisha maisha yake na maagizo ya Mungu, hata kama ingemgharim, hata kama isingeleta maana.

Wakati mwingine, kumfuata Mungu kunamaanisha kuachilia yale wengine wanayofikiria. Huenda kukamaanisha kujitoa muhanga kwa starehe au heshima. Hadithi ya Yusufu inatukumbusha kwamba imani ni zaidi ya kuamini tu. Ni tumaini linalowekwa katika matendo. Ni kuchagua njia ya Mungu, hata pale inapotugharimu vitu.

**Ni lini Mungu amekualika kuchagua utiifu badala ya starehe? Inaonekanaje unapomfuata Mungu na wakati wengine huenda wasielewe?**

*Bwana, nisaidie kusikiliza sauti yako hata kukiwa na kelele. Nipe nguvu ya kukufuata, hata kama itanigharimu kitu chochote. Amina.*

Wakati inakugharimu kitu.

# 15 Desemba

Mathayo 1:18-25, Isaya 30:21, Kumbukumbu la Torati 31:6

Mungu hakumwambia Yusufu afanye jambo rahisi. Alimwambia afanye lililo sahihi.

Kubaki. Kumchukua Maria kama mke wake. Kubeba uzito wa mashaka ya watu. Kuwa katika simulizi ambalo lingewachanganya wengine lakini lingetimiza kusudi la kiungu. Kuchagua utiifu badala ya urahisi, ujasiri badala ya starehe. Na kwa kufanya hivyo, akawa sehemu ya hadithi kuu zaidi kuwahi kusimuliwa.

Kwa macho ya tamaduni, uamuzi wa Yusufu kubaki mwaminifu kwa Maria ulionekana kama kitendo cha mtu mpumbavu, dhaifu, asiye na hamu ya kulinda jina lake au kuokoa mustakabali wake wa mbeleni. Lakini Yusufu aliamini zaidi kile Mungu alichosema katika utulivu wa usiku kuliko maoni yaliyosemwa na wengine wakati wa mchana.

Kuna nyakati ambapo Mungu hutuita tufanye mambo yasiyo ya starehe. Kuwafikia wengine ingawa ni rahisi kukaa kimya. Kusimama kwa ajili ya kweli ingawa kunahatarisha na kuwakera watu tunaowajali. Kuchagua ukarimu ingawa hali ya kifedha ni ngumu. Hofu hutufundisha kujilinda. Imani hutuita kuingia katika yasiyojulikana kwa utiifu wa kimya.

Kuna nyakati ambapo kumfuata Yesu hakuonekani kama ujasiri wa kishujaa, bali ni ugumu tu. Wakati ambapo hatutendi kwa sababu ya ujasiri mkubwa, bali kwa sababu hatuwezi kupuuza msukumo mpole wa Roho. Tunapotumia siku hizi katika uzoefu wa Yusufu, tukumbuke jinsi Mungu anavyowaheshimu wale walio tayari kuingia katika nafasi za udhaifu kwa jina lake. Pamoja na ahadi kwamba atakwenda nasi.

**Je, kuna sehemu ambayo Mungu anakuita ubaki palepale ambapo wengine wangetoka, uende pale ambapo wengine wasingeenda, kupenda pale ambapo wengine wangehukumu au kusema pale ambapo ukimya ungefaa zaidi?**

*Baba Mungu, mara nyingi unaniongoza katika maeneo yanayonitafakalisha au kunipa changamoto. Nipe ujasiri wa kukufuata, hata pale ambapo si rahisi au kunigharimu. Nifundishe kuamini njia zako ni za juu na mipango yako ni mizuri. Amina.*

# 16 Desemba

Mathayo 1:18-25, Waebrania 10:23

Yusufu alikuwa muumini wa Mungu wa Israeli. Muumini ambaye huenda alijua sheria kwa undani, hakika vya kutosha kuelewa uzito wa habari alizopokea. Maria alikuwa mjamzito. Na ingawa walikuwa wamepanga kuoana, hawakuwa wameoana bado. Wakati huo, kwa mwanamke kupatikana mjamzito kabla ya ndoa, sheria ilihukumu kifo kwa kupigwa mawe. Yusufu alijua kuwa hayo ndiyo yangemtokea kama adhabu.

Hofu ilimshinda Yusufu, hata kama kwa muda mfupi. Aliamua, labda kwa kuogopa hukumu, kukatishwa tamaa au aibu, kumwacha Maria kwa siri. Lakini mjumbe wa Bwana akaingilia kati.

Friedrich Nietzsche, mwanafalsafa wa Kijerumani, alipendekeza kwamba maadili, kama sehemu ya kanuni na taratibu, mara nyingi hutokana na hitaji la kudhibiti tabia na kuepuka matokeo mabaya. Hata hivyo, kwa wale wamjuao Mungu, maadili hutoka katika uzoefu wetu naye na kupokea zawadi zake zisizostahiliwa.

Martin Luther King aliwahi kusema: 'Ujasiri ni nguvu ya akili kushinda hofu.' Ndiyo, bila shaka, lakini ujasiri huu unatoka wapi? Kwa wale wanaomjua na kuupokea upendo wa Mungu wa dhabihu, ujasiri wetu unatoka kwake. Yusufu aliamini kwamba kile alichofunuliwa kwake katika ndoto kilikuwa cha kweli, kwamba mtoto aliyekabidhiwa Maria kwa Roho Mtakatifu alikuwa Mwana wa Mungu. Akiwa na imani hii, Yusufu alipata ujasiri katika Imani na kushinda hofu.

Mungu siku zote huwatia nguvu na moyo watu wake pindi wanapokabiliwa na majaribu. Maneno yake ni chanzo chetu cha tumaini na nguvu. Yusufu alipomtii Mungu, hofu zake zilitoweka. Tunapotenda kwa mujibu wa imani yetu, tukiwa na imani katika Mungu anayeweza kutusaidia kushinda, hofu hupoteza nguvu juu yetu.

Tunaposherehekea msimu huu wa Krismasi, Bwana na atusaidie kila mmoja wetu kushinda hofu zetu kupitia imani yetu kwa Yesu, Mwokozi.

**Je, unakabiliana vipi na hali ngumu katika maisha? Je, unaiacha hofu iongoze matendo yako, au unatafuta mwongozo na nguvu kutoka kwa imani yako? Ni nini unachohitaji leo kumwomba Mungu ili akupatie ujasiri wa kushinda?**

*Ee Bwana, nina imani kwako kwa changamoto ninazokutana nazo maishani ambazo hunifanya niogope. Naomba unisaidie kuzikabili, kuzishinda na kutokuhofu kupitia imani kwako. Amina.*

Meja Roy Samuel

Wakati inakugharimu kitu.

# 17 Desemba

Mathayo 1:18-25, Waebrania 11:7-8 na 24-27, 2 Samweli 6:14-22

Yusufu alichagua utiifu badala ya maoni ya watu. Alimchukua Maria kama mke wake si kwa sababu iliwiana na mawazo ya wengine, bali kwa sababu aliamini sauti ya Mungu.

Na hakuwa peke yake.

Nuhu alijenga safina wakati anga bado ni angavu. Musa alirudi Misri akiwa na kigugumizi na ujumbe ambao hakuna mtu aliyependa kuusikia. Daudi alicheza kwa furaha mbele za Bwana, hata wengine walipomkejeli. Mara kwa mara, waaminifu walikuwa tayari kuonekana wapumbavu machoni pa watu waliowazunguka.

Hofu ya kile ambacho wengine wanafikiri ni halisi. Kinaweza kutunyongonyesha, tusionekane, tukae kimya na kutuzuia kusema ‘ndiyo’ kwa kile Mungu akitakacho. Lakini imani haisubiri idhini ya kila mtu. Imani husonga mbele kwa ujasiri, hata pale inapo jitenga, kutoeleweka au kwenda kinyume na mkondo.

Kilicho muhimu zaidi kwa Yusufu hakikuwa sifa yake au nafasi yake katika jamii, bali heshima, ibada na tumaini alilomwekea Baba yake wa Mbinguni.

Je, ni hadithi gani Mungu anaweza kuwa anaandika kupitia utiifu wako?

**Je, hofu ya maoni ya wengine inakuzuia kusema ‘ndiyo’ kwa Mungu? Ni nini kingebadilika iwapo ungeamini kwamba sauti yake ndiyo yenye umuhimu zaidi?**

*Bwana, nisaidie kujali zaidi mwito wako kuliko kibali cha wengine. Ninapohofia kutoeleweka, nipe ujasiri kama wa Yusufu kutembea katika utiifu. Sauti yako iwe ndiyo inayoniongoza. Amina.*

# 18 Desemba

Mathayo 1:18-25, Isaya 41:10

Kuhamia nchi mpya hakukuwa tu kuhusu kupakia vitu vyangu. Bali pia ni hata mimi mwenyewe kujikana yaani kuachana na mambo ya zamani. Nililazimika kuanza shule upya katika mahali ambapo sikumjua mtu yeyote. Nilikuwa na hofu, pamoja na kwamba sikujionesha mara kwa mara. Kutengeneza marafiki wapya haikuwa rahisi, na kulikuwa na siku nilizotamani tu nirudi katika kile nilichohisi ni salama na nimekizowea.

Lakini wakati huo, Mathayo 1:18-25 ilinisaidia kukumbuka jinsi maisha ya Yusufu yalivyobadilika ghafla alipogundua kwamba Maria alikuwa mjamzito. Alijihisi kuchanganyikiwa na kuogopa kama nilivyohisi mimi. Lakini badala ya kukimbia, alimtumainia Mungu. Aya ya 24 inasema, ‘Yusufu alipoamka usingizini, alifanya kama vile malaika wa Bwana alivyomwagiza.’ Hilo liligusa moyo wangu. Yusufu hakuhitaji majibu yote ili kutii – alihitaji tu imani.

Hilo lilinifanya niulize nafsi yangu kama naweza kumtumainia Mungu hata nisipoelewa kwa nini nilipaswa kuhamia. Kisha nikakutana na Isaya 41:10: ‘Usiogope, kwa kuwa mimi nipo pamoja nawe; usifadhaike, kwa maana mimi ni Mungu wako.’ Ilinikumbusha kwamba hata kwenye eneo jipya, Mungu hakuniacha. Taratibu nilianza kumuona katika mambo madogo: mwanafunzi mwenzangu mwenye upole, tabasamu kanisani au mwalimu aliyenijali kwa dhati.

Sasa, naona kwamba mabadiliko haya yalikuwa sehemu ya historia yangu ambayo bado Mungu bado anaendelea kuiandika.

**Ni eneo lipi katika maisha yako sasa hivi unalohisi kutokuwa na uhakika au kutulia? Chukua muda kuzungumza na Mungu kuhusu hilo kwa uaminifu. Kisha iuliza nafsi yako: ‘Imani ingeonekana vipi hapa?’ Andika sala fupi au sentensi inayoonyesha uamuzi wako wa kumtumainia, hata kama njia iliyo mbele haieleweki.**

*Baba mwenye upendo, wakati mwingine ninahisi hofu, hasa mambo yanapobadilika ghafla. Nisaidie kukutumainia kama Yusufu alivyofanya. Nikumbushe kwamba mimi sipo peke yangu bali popote nilipo nawe upo. Asante kwa marafiki wapya na watu wema walioko karibu nami, kwa fursa mpya na kwa nafasi za kukua. Nisaidie kuwa na ujasiri wa kuchukua kila hatua kwa imani. Kwa jina la Yesu. Amina.*

Mandy Ambitan

# 19 Desemba

Mathayo 1:18-25, Isaya 43:1-2

Ulimwengu wa Yusufu ulibadilika ghafla kwa wakati mfupi. Kwa maneno machache tu, mustakabali aliokuwa ameuota kwa ajili yake na Maria ukaonekana kutowezekana. Hivyo akapanga mipango aliyodhani ni bora kwa kila mtu: kuvunja uhusiano wao na kuondoka kimya kimya. Lakini ndoa, mtoto na mustakabali vilikuwa sehemu ya mpango wa Mungu kwa familia hii isiyotarajia, hata kama Yusufu hakuweza kuiona bado katika ndoto, Mungu alimpa Yusufu kile hasa alichohitaji: uhakikisho na ujasiri wa kwenda hatua inayofuata.

Lakini tambua hili: utiifu wa Yusufu haukubadilisha hali yake. Bado kulikuwa na minong'ono na ukimya wa aibu, mashaka na kutokuelewana, mabishano na uhusiano uliovunjika. 'Ndiyo' yake haikumtoa katika hali ya kutokufurahia au mbali na kukataliwa, lakini ilimpeleka kwenye ufahamu wa karibu zaidi wa uwepo wa Mungu wake. Kusema 'ndiyo' kwa Mungu hakutabadilisha hali zetu kila mara au kutatua matatizo yetu, lakini kutatupeleka kwenye utegemezi wa kina zaidi na kutukaribisha karibu na yule anayeona picha yote.

Kama Yusufu, kutakuwa na nyakati ambapo mipango yetu tuliyoitengeneza kwa umakini inafumuka, tunapohisi kutokueleweka, tunapohofia kile ambacho wengine watafikiri, tunaposhindana na kukata tamaa. Katika nyakati hizo, tunaweza kujaribu kutafuta suluhisho sisi wenyewe, kutafuta njia ya kutoroka iliyo salama au yenye maana. Lakini mara nyingi ni katika mvutano huu kati ya hofu na imani, kati ya kudhibiti na kujisalimisha, ambapo Mungu anatualika tumwamini zaidi.

Hadithi ya Yusufu inatukumbusha kwamba hatutii kwa sababu njia ni rahisi. Tunatii kwa sababu ahadi hii ni ya kweli; ahadi inayosikika kwa sauti kubwa kuliko hofu yoyote na thabiti zaidi kuliko kutokuwa na uhakika wowote:

Mungu yupo pamoja nasi.

**Je, Mungu anakuuliza umtumainie katika jambo linalohisi kuwa na gharama kubwa sasa hivi? Ingeonekanaje kwenda hatua inayofuata kwa imani leo?**

*Mungu, ninashukuru sana kwa uwepo wako ulioahidiwa katika maisha yangu. Wakati wa kusema 'ndiyo' kwako kunaponigharimu kitu, nikumbushe kwamba wewe unastahili kila kitu. Nisaidie kukutumainia, hata njia inapokuwa haieleweki, na nipate amani si kwa matokeo bali katika uwepo wako. Amina.*

# 20 Desemba

Mathayo 1:18-25, Isaya 40:31

Kadiri wiki hii inavyokaribia mwisho, pumua kwa kina. Ondoka sehemu yenye kelele, shughuli nyingi, shinikizo na mbio – na upumzike. Leo, tunakualika upumzike katika uwepo wa upendo wa Baba yako wa Mbinguni, Yeye anayekuita kwa upole utoke kwa imani pamoja naye, hata kama inaweza kukugharimu chochote.

Majilio ni msimu wa kusubiri. Sio kusubiri kwa uvivu bali kungojea kwa utakatifu, kusubiri kwa tumaini. Kusubiri kwa kuamini kwamba Mungu anafanya kazi kivulini, katika utulivu, katika kile ambacho bado hajakikamilisha.

Kwa hiyo ruhusu nafsi yako ipumzike katika ukweli kwamba Emmanueli maana yake ni 'Mungu pamoja nasi'. Yuko karibu. Yeye ni mwaminifu. Yeye anatosha.

**Mungu anakuuliza umtumainie katika nini, hata kama inaweza kukugharimu? Tenga muda leo kukaa kimya mbele zake. Katika utulivu, mwombe Mungu akutane nawe hapo. Pokea amani yake. Ruhusu ujasiri wake ujaze moyo wako. Unaposikiliza, chukua hatua moja ya imani unayoamini, umeitwa kuchukua wiki ijayo na muombe akupatie nguvu ya kuichukua.**

*Bwana, nakushukuru kwa mfano wa Yusufu – mtu ambaye alitii na kuamini kwamba njia yako ndiyo bora. Nisaidie kubeba ujasiri huu katika maisha yangu mwenyewe, kuchagua imani badala ya hofu ya gharama. Nijaze kwa amani na uwepo wako ninaposubiri kwa matarajio kuja kwa Yesu. Shikilia roho yangu ikiwa laini, hatua zangu ziwe za uaminifu na macho yangu yaelekezwe kwako. Amina.*


Mchungaji:
Wakati Imani Inapong'aa Kupitia Hofu

# 21 Desemba

Luka 2:8-20

Mchungaji hakuwa na hadhi kubwa machoni pa jamii. Walikuwa wakifanya kazi zao, wakilinda kondoo usiku kwa utulivu, wakati ghafla kila kitu kikabadilika. Malaika alijitokeza na utukufu wa Bwana ukaangaza mbinguni. Biblia inasema walihofu sana. Ni nani asingehofia?

Lakini kisha yakaja maneno yanayotokea mara nyingi katika hadithi ya Krismasi: 'Msiogope.' Malaika alileta ujumbe wa habari njema, siyo kwa wenye nguvu au wenye nafasi, bali kwa watu wote, akianzia na wale waliokuwa pembezoni.

Wakati huo, wachungaji wangeweza kuruhusu hofu iwazuie. Lakini hawakufanya hivyo. Majibu yao yalijaa imani. Hawakusubiri hadi wapate majibu yote.

Hawakurusu hofu au kutokuwa na uhakika au kukata tamaa. Walienda mara moja kuona kile Mungu alichokuwa amefanya. Na baada ya kumuona Yesu wao wenyewe, walitoa taarifai hizo kwa furaha.

Hadithi hii inatufundisha kwamba hofu ni sehemu ya kawaida ya maisha, hata Mungu anapofanya jambo jema. Lakini imani inaweza kung'aa katikati ya hofu zetu. Tunapochagua kusikiliza sauti ya Mungu, tunapochukua hatua inayofuata ya uaminifu, tunajifungulia furaha na kusudi.

Wachungaji walikuwa mashahidi wa kwanza wa kuzaliwa kwa Yesu, si kwa sababu walikuwa jasiri au muhimu, bali kwa sababu walikuwa katika imani.

**Wakati hofu inapojaribu kukuzidi nguvu, unawezaje kuruhusu imani iangaze? Ni habari njema gani Mungu anakuomba uibebe katika maisha yako na maisha ya wengine?**

*Mungu,nisaidie nuru yako iangaze katikati ya hofu zangu leo. Nipe imani inayonisogeza mbele kwa tumaini na furaha. Amina.*

# 22 Desemba

Luka 2:8-20, Isaya 9:2, Yakobo 2:5

Ilikuwa ni usiku wa kawaida kwa wachungaji – baridi, ukimya, wa kawaida. Wanaume hawa hawakuchukuliwa kuwa watu wenye nguvu au muhimu, bali wafanyakazi wanyenyekevu waliokuwa wakifanya kile walichozoea kila siku: kulinda makundi yao ya kondoo usiku. Kisha ghafla, kila kitu kikabadilika.
Mbingu zikaangaza kwa utukufu.
Malaika wakaja na ujumbe.
Wakati uliojaa hofu.

Wachungaji waliogopa sana, na kwa kweli walikuwa na sababu ya kuogopa! Hii haikuwa aina ya tukio walilolitarajia. Lakini maneno ya kwanza ya malaika yalikatiza hofu ile, maneno tunayoyasikia mara nyingi katika Maandiko: 'Msiogope.'

Ni kauli ile ile iliyonenwa kwa Zakaria, kwa Maria, kwa Yusufu. Tena na tena, Mungu akiwalika watu kuachilia hofu zao, kwa maana jambo takatifu lilikuwa linatokea.

Habari njema ya furaha kuu kwa watu wote. Kwa mikono iliyokuwa ikitetemeka na mioyo iliyokuwa ikipiga kwa kasi, wachungaji waliacha mashamba yao na kukimbilia kuona jambo hili lililotokea. Hawakusubiri hadi hofu ipite au mshangao upungue – walichukua hatua.

Imani haimaanishi kwamba hatutakuwa na hofu. Inamaanisha kwamba tunamwamini Mungu vya kutosha kuendelea mbele.

Katika Maandiko yote, tunaona aina hii ya utiifu wa kishujaa. Esta alimkaribia mfalme akijua maisha yake yako hatarini. Danieli aliendelea kuomba hata pale simba wenye njaa walipomsubiri. Maria alisema 'ndiyo' kwa Mungu kabla hajajua gharama yake. Kila mmoja wao alikabiliana na hofu, lakini imani ikaangaza njia.

Wachungaji hawa wanyenyekevu wanatufundisha kwamba hofu inaweza kuwa sehemu ya hadithi yetu, lakini si lazima iwe mwisho wake. Waliacha mashamba yao ili kukutana na Yesu na walirudi wakimtukuza Mungu. Walibadilishwa milele.

Ni nini kingeweza kutokea kama nasi, kama wao, tungeacha imani iangaze katikati ya hofu?

**Ni wapi hofu inakuzuia sasa hivi – na ingeonekanaje kuchukua hatua hata hivyo?**

*Mungu wa nuru na tumaini, asante kwa kukutana nasi kwa nyakati za kawaida. Katika nyakati za kawaida za leo, acha imani yangu iangaze kuliko hofu yangu ili nikutukuze katika kila nifanyalo. Amina.*

# 23 Desemba

Luka 2:8-20, 2 Wakorintho 5:7

Nilipokuwa na umri wa miaka 21, niliruka kwa bungee kutoka daraja lililokuwa juu ya Mto Kawarau karibu na Queenstown, New Zealand. Kabla ya kuruka, taulo dogo liliwekwa kwenye vifundo vya miguu yangu likishikiliwa kwa kamba nyembamba, kisha kamba ya bungee ikaunganishwa. Nilijiuliza, 'Basi tu?' 'Hiyo ndiyo ninayohitaji?' 'Hakuna kingine zaidi?' Ni kuruka tu. Sijawahi kuweka imani kubwa zaidi kwa taulo kuliko siku hiyo!

Tunaweza kuchagua kupata hofu tuliyoijiletea wenyewe kupitia mambo ya kutafuta msisimko kama kuruka kwa bungee. Lakini mara nyingi zaidi, hofu huja bila kutarajiwa, wakati ambapo hatutarajii kabisa, ikigusa maeneo ya ndani kabisa ya fahamu zetu, na wakati mwingine ikileta hisia kali sana na hata mwitikio wa mwili. Lakini sio yote mabaya. Hofu ni mfumo wa asili wa kujilinda unaotuzuia na madhara au bahati mbaya wakati fulani. Hata hivyo, jinsi tunavyojibu hofu kwa mwanga wa imani yetu ndilo jambo la muhimu sana.

Wachungaji waliunganishwa ghafla na malaika wa Bwana – aliyekuja na habari njema ambayo ingesababisha furaha kuu kwa watu wote – na walihofia sana! Na kana kwamba kusisitiza jambo hilo – na kuongeza hofu ya wachungaji – malaika huyo akaunganishwa ghafla na jeshi kubwa la malaika wengine, nao walikuwa wakimsifu Mungu na kusema: 'Utukufu kwa Mungu juu mbinguni, na amani duniani kwa wale wanaompendeza Mungu' (Luka 2:14). Jibu la wachungaji kwa tukio hili la kiroho lilikuwa nini? Walijibu, twendeni tukalione jambo hili lililotokea, ambalo Bwana ametujulisha' (Luka 2:15).

Kama kuruka kwa bungee, katika maisha ya imani, wakati mwingine tunajikuta tukiuliza maswali haya: 'Basi tu?' 'Hiyo ndiyo ninayohitaji?' 'Hakuna kingine zaidi?' Maswali haya huenda yanatokana na dhana kwamba lazima kuwe na jambo la ziada kutoka kwetu zaidi ya imani tuliyoonyesha kwa Kristo na neema isiyostahiliwa ya Mungu ambayo tayari imeonyeshwa kwetu.

Kwa hakika, kilichobaki kwetu kufanya ni kuendelea kuchukua hatua ya imani kutoka katika hofu au mambo yasiyojulikana na kuingia katika yale ambayo Mungu anatualika kila siku, jambo linalowezekana tu kwa kupitia ujio wa Kristo katika ulimwengu wetu – upendo wa kweli kati yetu.

Meja Daniel Templeman Twells

# 23 Desemba

Luka 2:8-20, 2 Wakorintho 5:7

Ni nini mwitikio wako wa asili kwa hofu katika maisha yako?

Ni nini kinakuruhusu kukabiliana na hofu kwa mtazamo wa imani na kuishinda?

Ni nini kinakuzuia kufanya hivyo?

Kuchukua 'hatua ya imani' kunaonekanaje kwako katika hali yako ya sasa?

*Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, Upendo ulio kati yetu,*
*Upendo mkamilifu unaofukuza hofu yote.*
*Nuru ya ulimwengu, tuitie kutoka kwenye sehemu zenye hofu na giza,*
*Tutoke katika kutojua na kuingia katika uwazi wa kimungu.*
*Hofu ibadilike kuwa imani, giza liwe nuru,*
*Tujulishe siri ya ndani ya Majilio na Upatanisho,*
*Tungojee katika sehemu ulizotuita, ambapo bado hatujafika.*
*Nuru na Uzima wa ulimwengu, iwe hivyo.*
*Amina.*

Meja Daniel Templeman Twells

# 24 Desemba

Luka 2:8-20, Yohana 1:14

Leo, tunakualika usimame, upumzike katika uwepo wa Baba yako wa Mbinguni.
Yeye aliyefanyika mwili na kukaa kati yetu.
Yeye aliyehama na kuishi miongoni mwetu.
Yeye aliyekuwa Emanueli, Mungu pamoja nasi.
Ukaribu wake ujulikane kwako leo.
Upumue kwa kina katika uwepo wake.
Na uwepo wake uwe zawadi yako kuu zaidi Krismasi hii.

**Ni wapi zaidi unahitaji kuupokea uwepo wa Emanueli, Mungu pamoja nawe, leo?**

*Yesu, asante kwa kuja karibu, kwa kuingia katika ulimwengu wetu na katika hofu zetu. Katika utulivu wa siku hii, nisaidie kupunguza mwendo na kukumbuka kwamba uko hapa. Wakati wasiwasi unapoibuka au kutokuwa na uhakika kunapodumu, acha imani iangaze katikati ya hofu yangu. Nikumbushe kwamba wewe ni Emanueli, Mungu pamoja nasi, na kwamba uwepo wako unaleta amani ambayo hakuna hofu inayoweza kutikisika. Nisaidie kukutumainia leo na kupumzika katika nuru ya upendo wako. Amina.*



Siku ya Krismasi:

# Imani Inayoleta Amani

# 25 Desemba

Isaya 9:1-6, Yohana 14:27

Siku ya Krismasi, tunasherehekea kuzaliwa kwa Yesu. Siyo tu kama mtoto mchanga ndani ya hori, bali kama Mwokozi anayebeba amani kwa ulimwengu uliojaa hofu. Muda mrefu kabla ya Msalaba au kaburi tupu, amani ilikuja ikiwa imefungwa kwa nguo za kitoto na kulazwa mahali pa unyenyekevu. Yesu, Mkuu wa Amani, alikuja karibu.

Miaka kadhaa baadaye, aliwaambia wanafunzi wake: ‘Amani nawaachieni; amani yangu nawapa. Siwapi kama vile ulimwengu utoavyo. Mioyo yenu isifadhaike wala msiwe na hofu’ (Yohana 14:27).

Amani anayotoa Yesu si kitu ambacho ulimwengu unaweza kutoa. Haitegemei hali tulivu au majibu yaliyo wazi. Ni tumaini la kina na imara kwamba Mungu yupo pamoja nasi, hapa, sasa hivi.

Krismasi haifuti hofu zote, lakini inatukumbusha ni wapi tunaweza kuweka tumaini letu. Ujumbe ulioanza na ‘Msiogope’ bado ni ujumbe ambao Mungu anachagua kunipa leo. Sitembei peke yangu. Mungu amekuja karibu. Emanueli, Mungu pamoja nasi, bado ni ukweli leo.

Kuchagua imani badala ya hofu kunamaanisha kuikaribisha amani hiyo mioyoni mwetu. Kunamaanisha kuamini kwamba Yesu yupo katika furaha na pia katika mapambano, na kuruhusu amani yake iunde jinsi tunavyoishi, jinsi tunavyotumaini na jinsi tunavyoukabili ulimwengu unaotuzunguka.

**Ni hofu zipi unataka kumkabidhi Yesu leo? Amani yake inaweza kukusaidiaje kuishi kwa imani katika siku zijazo?**

*Yesu, asante kwa kuja katika ulimwengu wetu na katika maisha yangu. Nijaze kwa amani yako leo na unisaidie kuchagua imani badala ya hofu kila siku. Amina.*

JESHI LA WOKOVU

Mfululizo huu unajumuisha tafakari zilizoandikwa na Kamishna Patti Niemand na Ashleigh Pringle wa Jeshi la Wokovu Kimataifa kwenye idara ya Maisha ya kiroho, pamoja na waandishi wageni kutoka sehemu mbalimbali za dunia. Kwa maelezo zaidi juu ya maendeleo ya Maisha ya Kiroho Kimataifa ya Jeshi la Wokovu, tembelea salvationarmy.org.

Nukuu za Maandiko Matakatifu zimechukuliwa kutoka:
Biblia Takatifu, Toleo la Kimataifa Jipya® NIV® Haki miliki © 1973, 1978, 1984, 2011 na Biblica, Inc. Imetumika kwa ruhusa. Haki zote zimehifadhiwa duniani kote.
Biblia Takatifu, Toleo la Tafsiri Hai Mpya, haki miliki © 1996, 2004, 2015 na Tyndale House Foundation. Imetumika kwa ruhusa ya Tyndale House Publishers, Inc., Carol Stream, Illinois 60188. Haki zote zimehifadhiwa.
Biblia Takatifu, Toleo la Kawaida la Kiingereza. ESV® Toleo la Maandishi: 2016. Haki miliki © 2001 na Crossway Bibles, huduma ya uchapishaji ya Good News Publishers.